

Jina.....Nambari ya Mtahiniwa...../.....

102/2

Sahihi ya Mtahiniwa.....

KISWAHILI Karatasi ya 2 LUGHA

JULAI/AGOSTI 2014

Tarehe.....

Muda: Saa 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA UPILI ZA WILAYA YA NAKURU

Maandalizi kwa Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

- Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali **yote**.
- Majibu yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi hizi za maswali.
- Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye mkusanyiko huu wa karatasi.
- Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.**
- Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

Kwa matumizi yam tahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1.UFAHAMU (Alama 15)

Matumizi ya sheng' yameshamiri sana nchini Kenya hata miongoni mwa vijana. Ni kilugha ambacho kinakisiwa kuzuka katika miaka ya 60 na 70 katika makazi ya mashariki mwa jiji la Nairobi kama vile Kaloleni, Mbotela, Bahati na kadhalika.

Kwa sasa ni kilugha kilichoenea kwingi nchini Kenya na kuwa kitambulisho cha takriban vijana wengi. Wataalamu mbalimbali wanabainisha nadharia mbalimbali kuhusu chanzo cha lugha hii. Kuna nadharia mbili kuu kuhusu asili ya lugha ya Sheng; kwamba kilugha hiki kiliibuka kutokana na wahuni na wakora jijini Nairobi ambao lengo lao lilikuwa kuwasiliana kwa siri. Nadharia nyingine ni kuwa kilichipuka kutokana na vijana ambao walizua lugha ya kuwasiliana baada ya uhuru kwa sababu walikichukia Kiswahili ambacho walikiona kama lugha ya uboi.

Dhana hizi kwa muda mrefu, zimeathiri mitazamo kuhusiana na kilugha hiki. Kwa sasa ni kilugha ambacho kinasambaa katika sehemu mbalimbali za Kenya na watu wa matabaka mbalimbali wanakitumia. Kilugha hiki kimeanza kuashiria uhalisia mkubwa wa maisha ya kisasa, zaidi katika jamii ya Wakenya. Aidha, sheng imejitanzua kutoka hali ya kuwa kilugha cha maongezi pekee na sasa kinatumiwa katika baadhi ya vitabu, hata waandishi wa vitabu wameanza kukitumia, kwa mfano katika miaka ya 80, David Mailu katika kitabu chake 'Without Kiinua Mgongo' alitumia sheng.

Katika siku za hivi karibuni, Riwaya ya 'Kidagaa Kimemwozea' iliyoandikwa na Ken Walibora kilugha cha sheng kimepewa nafasi kama kitambulisho cha vijana kupitia kwa mhusika DJ Bob. Vilevile kumezuka vyombo vya habari kama redio, mfano idhaa ya Ghetto, redio ambayo inaendeleza mawasiliano kwa matumizi ya sheng. Kuna vipindi na matangazo ya kibiashara katika runinga ambayo yanaendelezwa kwa sheng. Kwa mfano katika gazeti la Taifa Leo, kuna ukumbi wa 'Mchongoano' ambao umekuwa ukiendelezwa kwa Sheng.

Nchini Kenya ambapo asilimia 60% ya idadi ni vijana, Sheng imetokea kuwatambulisha vijana. Katika enzi hii ya **Teknohama**, wanaomiliki vyombo vya habari na sekta nyingine za biashara wamegundua kuwa matumizi ya Sheng ndiyo njia mwafaka zaidi ya kulifikia soko kubwa la vijana kwa ajili ya kueneza matangazo ya bidhaa na huduma za kibiashara. Kwa hivyo, Sheng imekuwa daraja la kuwafikia na kuwavutia vijana.

Hata hivyo, kwa upande mwingine matumizi ya Sheng yamelaumiwa na walimu wengi katika shule za msingi na zile za upili kuwa ni sababu mojawapo kuu ya kushuka kwa matokeo ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza miongoni mwa wanafunzi. Sheng imelaumiwa kwamba inasababisha wanafunzi kutozingatia mafunzo ya kanuni za sarufi na tahajia au maendelezo. Wataalamu wanadai kuwa ni **msimbo** ambao hauzingatii sheria za sarufi na tahajia kwa sababu zizizofahamika, kwani ingawa muundo wake wa kisarufi hushahabiana na ule wa Kiswahili, Sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake.

Ingawa sheng imekuwa ikipigwa vita, kuna wataalamu ambao wana mtazamo kwamba juhudi hizo hazizuiwi kufanikiwa kwani sheng ni chombo cha mawasiliano miongoni mwa vijana na kwa hivyo ina umunimu wake ambao hauwezi kufumbiwa macho. Wanasema kuwa ni chombo ambacho kinafumbata hisia na mshikamano wa kizazi kipya kama ilivyojitokeza katika kauli mbiu ya mgombeaji urais mwaka wa 2012, 'Tunawesmake'.

Katika hali ambapo kiwango cha ubora wa matokeo ya Kiswahili **yalidorora** katika mtihamu wa Kidato Cha nne (KCSE) mwaka wa 2012 na kuwa asilimia 35.81 pekee yakilinganishwa na asilimia

48.82 ya mwaka 2011, sheng imekuwa ikilatumiwa kuwa ndicho chanzo cha kudorora kwa viwango vya ubora wa matokeo. Baadhi ya hao wataalamu wanasema kwamba sheng haipaswi kuhujumiwa, kinachohitajika kufanywa ni kuwaelimisha vijana kuhusu mipaka ya matumizi yake.

(a) Taja mada ya kifungu hiki. (alama 1)

.....
.....

(b) Fafanua nadharia mbili zilizoeleza asili ya lugha ya Sheng. (alama 2)

.....
.....
.....

(c) Eleza matumizi bainifu ya kilugha cha Sheng katika jamii ya sasa. (alama 3)

.....
.....
.....

(d) Taja matokeo hasi ya matumizi ya Sheng katika jamii. (alama 3)

.....
.....
.....

(e) Ni kwa nini mwandishi Walibora ameshirikisha matumizi ya Sheng katika kazi yake ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 2)

.....
.....
.....

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu hiki. (alama 4)

i) Teknohama

.....

ii) Kudorora

.....

iii) Msimbo

.....
iv) Kuhujumiwa.
.....

2. UFUPISHO

Kuna dhana nchini ambayo inazidi kuenezwa miongoni mwa vijana na usipochunga, tutakuja kujipata pabaya katika siku za usoni. Kwa kipindi cha miongo miwili hivi iliyopita, sekta ya sanaa nchini imekuwa ikiimarika kwa kasi. Kuna wasanii ambao wamefanikiwa kujiendeleza kimaisha kutokana na talanta zao lakini pia kuna wale ambao wamebaki katika hali ya uchochole, pengine kutokana na kuwa hawafahamu vyema jinsi ya kujisimamia na kutumia talanta zao kama mbinu ya kujipatia riziki. Kwa muda huo wote, vijana wengi Wamejikuta wakivutiwa mno na hali ya kimaisha ya wasanii walioboea, hasa wanamuziki, na hivyo basi hujitosa kwenye sekta ya sanaa wakiwa na matumaini makubwa ya kuishi maisha ya kifahari.

Imefikia kiwango ambapo washikadau wa masuala ya kuendeleza maisha ya vijana, ikiwemo Wizara ya Michezo, Vijana na Utamaduni wanawekeza pakubwa kuendeleza sekta ya sanaa. Ni hapa ndipo wasiwasi unaibuka kwa kuwa huenda tukachukulia Kwamba juhudi za kuwezesha vijana kujikimu kimaisha zitafanikiwa tu iwapo sekta ya sanaa itaimarishwa. Dhana hii ni potovu na ni sharti washikadau wazinduke, waanze kupanua mawazo yao na kuwa na busara kwenye hatua wanazochukua ikiwa wana nia ya kuwezesha vijana kujikimu kimaisha na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Ukichunguza kwa makini, utapata kuwa ni asilimia ndogo mno ya wanaojitosa kwenye sanaa ambao wanaweza kusemekana wana ari na kipawa cha kutosha kuweza, kuchangia ipasavyo kwenye uchumi wa kitaifa kwa kutumia vipawa hivyo. Hivyo basi, suala ibuka ni je, asilimia kubwa iliyosalia huwa wanafanya nini, na ni jinsi gani wanavyoweza kuwezesha wajiendeleza zaidi kimaisha? Hapatakuwa na haja ya kuwekeza mamilioni ya pesa katika kuendeleza sekta ambapo mapato yake hayatakuwa yenye faida kwa taifa.

Humu nchini tumekuwa na tabia ya kupuuza sekta zilizo muhimu sana, na matokeo yake ni kuwa tunaishia kuagiza bidhaa kutoka nje ilhali tungeweza kujitengezea wenyewe nchini. Baadhi ya yale tuliyopuuza ni useremala, ushonaji wa nguo, utengezaji wa bidhaa za ngozi na hadi miaka ya hivi majuzi, kilimo kilikuwa kimezikwa kwenye kaburi la sahau miongoni mwa vijana. Ni kutokana na hali hii ambapo vijana wengi wanaochukua mikopo kutoka kwa hazina waliotengewa na Serikali huwa hawafanikiwi, kwa kuwa hakuna uwekezaji wa kutosha uliowekwa kuimarisha ujuzi wao wa kibiashara.

Kwa sasa, Serikali iko katika harakati za kuagiza vipakatalishi kutoka India. Na kumbuka vyema serikali ilivyotangaza kuwa vipakatalishi vitakuwa vikitengezwa nchini. Kwa kuviagiza kutoka mataifa ya kigeni, ni wazi kuwa hatujafikia kiwango cha kujitengezea vifaa hivyo kwa kiwango kikubwa, ingawa kuna watu kadha ambao huagiza vipuri na kujitengezea kompyuta wenyewe. Vijana wanahitaji kuwezesha katika nyanja zote, na wala sio kwa sanaa na michezo pekee.

Iwapo tutaendelea kutoa picha ya kuwa ni michezo na sanaa, pekee zilizo muhimu kwa vijana, itafika wakati ambapo tutaanza hata kuagiza mboga kutoka mataifa ya nje tusipojihadhari. Bila shaka tuna nafasi ya kurekebisha mienendo yetu, na ni vyema ikiwa tutachukua hatua hiyo ha raka iwezekanavyo.

(a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 90 – 95. (alama 8, 1 ya Utiririko)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Nakala safi.

.....
.....
.....
.....

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Kwa kutumia maneno 70 – 75, eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 5, 1 ya Utiririko.)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....
.....
.....
.....

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Taja sauti mbili zenye sifa zifuatazo za matamshi.

i) Mbele, wastani, tandazwa. (alama 1)

ii) Kati, chini, tandazwa. (alama 1)

b) Bainisha viambishi na mzizi katika neno kunipa. (alama 3)

c) Huku ukitoa mfano mmoja mmoja bainisha makundi matatu ya vivumishi vya sifa.

(alama 3)

i)

ii)

iii)

d) Huku ukipiga mstari, tunga sentensi moja yenye chagizo na yambwa. (alama 2)

e) i) Kirai ni nini? (alama 1)

ii) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo.

Walimu hao hufunza wanafunzi kwa bidii. (alama 2)

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.

Kitabu alichokinunua juzi kina uzuri mwingi. (alama 4)

.....
.....
.....

.....

.....

.....

.....

.....

g) Huku ukitoa mfano mmoja mmoja, eleza namna tatu za kukanusha hali ya **KU**. (alama 3)

- i)
- ii)
- iii)

h) Andika wingi wa ukubwa wa sentensi ifuatayo.
Huyu ndiye mwanamume mwembamba zaidi. (alama 2)

.....

i) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi.
Mwalimu alisema angemwadhibu mwanafunzi siku iliyofuata. (alama 2)

.....

j) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.
Mtamba yule amekula nyasi nyingi. (alama 1)

.....

k) Kanusha sentensi ifuatayo kwa umoja. (alama 1)
Walipochekesha watu walipelekwa ng'ambo.

.....

l) Eleza maana tatu za sentensi ifuatayo. (alama 3)
Wakenya hawakienzi Kiswahili kama Watanzania.

.....

.....

m) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa nomino. (alama 2)
Mlachake **alilewa** hata akashindwa kutembea.

.....

n) Tumia neno **makini** kama kitenzi katika sentensi. (alama 1)

.....

o) Sahihisha sentensi ifuatayo. (alama 2)

Wasee hao waliwaambia wamama wale kuwa hawakuwa na kizazi nao hata baada ya kuwatusi vibaya.

.....
.....

p) Tunga sentensi katika wingi ukitumia nomino hizi pamoja na kisisitizi mwafaka. (alama 2)

i) noti

.....
.....

ii) kiziwi

q) Tunga sentensi ukitumia **ni** kama:

i) Swali au kiulizi. (alama 2)

.....
.....

ii) Amri

r) Tunga sentensi ukitumia neno labda kudhihirisha maana zifuatazo. (alama 2)

i) Shaka

.....
.....

ii) Uwezekano.

4. ISIMUJAMII (Alama 10)

Utafiti wa kiisimu, Fasihi Simulizi na mapisi unaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika. Fafanua. (alama 10)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA